

A WOTE NI WADHAMBI. Warumi 3:10-18, 21-32.

- ❖ Tu wadhambi na hatuwezi kuchagua kutenda mema.
- ❖ Roho Mtakatifu ndiye pekee anayetengeneza...
 - Ushawishi kuwa tu wadhambi.
 - Kuondoa kiburi.
 - Shauku ya kumwendea Yesu ili kupata msamaha.
 - Badiliko katika Maisha yetu.

B WASIO WAUMINI. Warumi 1:22-27.

- ❖ Maneno hayo yanaaksi kila tunachosoma kwenye magazeti na kuona kwenye taarifa za habari.
 - Sanamu za watakatifu, wanayama.
 - Kujifanyia miungu katika nafsi zetu, michezo, sinema mitindo na watu maarufu...
 - Kuenea kwa wapenzi wa jinsia moja.
 - Ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa.
- ❖ Tangu dhambi ilipoonekana duniani, mwanadamu amekuwa muovu na amemkimbia Mungu. Suluhisho pekee kwa kila mwanadamu ni kumpokea Yesu kama Mwokozi wake binafsi.

C WAUMINI. Warumi 2:1-3, 17-24.

- ❖ Waumini hujivunia kwa kutokuwa kama “wapagani” na kuwahukumu. Hata hivyo, waumini wanatenda dhambi sawa na wasioamini.
- ❖ Mungu huwahukumu waumini, pia. Anadai zaidi kutoka kwao, kwa sababu wa maarifa ya kweli zake zaidi kuliko wasioamini.
- ❖ Suluhisho pekee kwa waumini ni kujisalimisha kwa Mungu kila wakati katika Maisha yao.
- ❖ Waumini na wasioamini, waume kwa wake, matajiri na masikini... Sote tu wadhambi na tunakabiliwa na adhabu.
- ❖ Kusingekuwa na tumaini kwa yeyote kama si neema ya Mungu.

D SULUHISHO LA MUNGU KWA WADHAMBI. Warumi 1:16-17.

- ❖ Haki ya Mungu humaanisha kuwa kila aliye na imani katika injili (Kifo cha Yesu msalabani) atapata wokovu.
- ❖ Unapoamini katika kifo cha Yesu kwa imani, ni imani hiyo hukuongoza kumwamini Mungu zaidi na zaidi. Tuna uzima na kuitwa wenye haki kwa imani hiyo.

E TOBA. Warumi 2:5-10.

- ❖ Mdhambi anaweza kung'ang'ania wokovu alioutoa Mungu (kifo cha Yesu) kwa imani. Imani hiyo huongoza katika toba na badiliko katika maisha yake.
- ❖ Wadhambi wanaotubu huwa na mtazamo mzuri.
- ❖ Wadhambi wasiotumbu hutenda maovu.